MWANANCHI.CO.TZ
IJUMAA FEBRUARI 5, 2021
MWANANCHI

# Afya


**Mchaichai hupunguza dalili zinazotokana na Covid 19** UK 19

**Wanawake waeleza faida ya kumnyonyesha mtoto miezi sita** UK 21



**NAMNA YA KUTIBU CHANGAMOTO YA KIGUGUMIZI** UK 20-21 >

# JINSI DAWA ZA KULEVYA ZINAVYOCHANGIA MAGONJWA HATARI YASIYOAMBUKIZA



**41 milioni**

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) magonjwa yanayosumbua zaidi ni kisukari, saratani, matatizo ya moyo, shinikizo la damu na selimundu ambayo huchangia vifo zaidi ya milioni 41







Elizabeth Edward, Mwananchi
eedward@mwananchi.co.tz

Wakati kasi ya magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza ikizidi kuongezeka nchini na mfumo wa maisha ukitajwa kuwa chanzo kikuu, matumizi ya dawa za kulevya nayo yametajwa kuchangia kuongezeka kwa magonjwa hayo.

Takwimu za wizara ya afya zinaonyesha kitaifa tatizo la magonjwa yasiyo ya kuambukiza linaongezeka kwa kasi, ongezeko likiwa asilimia 24 ndani ya miaka miwili na yakichangia vifo takriban asilimia 33 hadi 35.

INAENDELEA UK.18

INATOKA UK.17



# Jinsi dawa za kulevya zinavyochangia magonjwa hatari yasiyoambukiza

Magonjwa yanayosumbua zaidi ni kisukari, saratani, matatizo ya moyo, shinikizo la damu na selimundu ambayo kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) yanachangia zaidi ya vifo milioni 41.

Maandiko mengi ya wataalamu yamekuwa yakieleza kuwa kwa kiasi kikubwa magonjwa haya husababishwa na mtindo mbovu wa maisha ukihusisha ulaji wa vyakula vyenye mafuta, sukari na wanga mwingi.

Sababu nyingine kutofanya mazoezi pamoja na kutokuwa na utamaduni wa kufanya vipimo na kugundua tatizo mapema kisha kulipatia matibabu katika hatua za awali.

Chanzo kingine ambacho kiKatika mahojiano na gazeti hili Kamishna Msaidizi wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (CDEA), Dk Cassian Nyandindi anasema matumizi ya dawa za kulevya yamekuwa yakichangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza.

"Dawa za kulevya ni kemikali ambazo mtu akizitumia zinakwenda kuathiri mfumo wa fahamu hasa ubongo. Athari hizi zinaweza zisionekana kwa haraka hadi pale mtumiaji atakapokuwa na mabadiliko ya kitabia, kimwonekano na hata matendo yake.

"Dawa hizi zina utofauti pia kwa namna zinavyoleta madhara mwilini, cocaine na mirungi husababisha mifumo ya mwili kufanya kazi juu ya kiwango, hapa inahusisha mapigo ya moyo, msukumo wa damu hivi vyote vinalazimishwa kufanya kazi kwa kiwango cha juu zaidi ambayo ni hatari," alisema Dk Nyandindi na kuongeza

"Heroin au vipumbaza husababisha mifumo ya mwili kufanya kazi chini ya kiwango, mfano binadamu wote tunapumia na kikawaida inatakiwa iwe ni mara 16 hadi 20 kwa dakika moja, sasa mtu anayetumia kipumbaza kama heroin na bangi atakuwa anapumia chini ya kiwango hicho, hata shinikizo lake la damu linakuwa chini zaidi,".

Anasema madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya yanaweza kumsababishia mtumiaji kupata magonjwa yasiyoambukiza mfano matatizo ya figo, mshtuko au shambulio la moyo na hata shinikizo la damu.

Kulingana na mtaalamu huyo hilo linatokana na ukweli kwamba dawa za kulevya zinapoingia kwenye mwili wa binadamu uchakataji wake unafanyika kwenye ini, figo na moyo, viungo ambavyo kwa kiasi kikubwa ndivyo vinashambuliwa na magonjwa yasiyoambukiza.

**NUKUU**

**"Dawa hizi zina utofauti pia kwa namna zinavyoleta madhara mwilini, cocaine na mirungi husababisha mifumo ya mwili kufanya kazi juu ya kiwango, hapa inahusisha mapigo ya moyo, msukumo wa damu hivi vyote vinalazimishwa kufanya kazi kwa kiwango cha juu zaidi ambayo ni hatari."**

**Dk Nyandindi**

Dawa hizi unapozitumia zinakwenda kufanya kazi kwenye figo, ini na moyo. Mfano mtu akitumia cocaine uchakataji wake unafanyika kwenye moyo, uchafu utatoka kupitia figo, effect yake ya kuongeza pumping inaenda kufanyika kwenye moyo.

"Mtu anapokwenda kwa daktari anaelezea shida yake ya moyo au figo bila kuweka wazi kuwa amewahi kutumia dawa za kulevya, hata daktari anayemtibu ataangalia ule ugonjwa na ndiyo hapo unasikia magonjwa yasiyoambukiza yameongezeka kumbe ukifuatilia kuna ambao yamesababisha na matumizi ya dawa za kulevya,"

Mbali na hayo, madhara mengine ni kifua kikuu hasa kwa watumiaji wa bangi, homa ya ini kutokana na kuchangia sindano, matatizo ya akili hata kuchangia kwenye maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutokana na kuchangia sindano na kufanya ngono zembe.

Kwa mujibu wa kamishna huyo ambaye pia ni daktari bingwa wa magonjwa ya akili na dawa za kulevya kuna athari nyingi za kiafya zinazosababishwa na matumizi ya dawa hizo.

Daktari huyo alieleza kuwa matumizi hayo huchangia katika kusababisha mishipa ya damu kupasuka, kupata kiharusi, kutokwa na damu puani na vifo vya ghafla ambavyo husababishwa na kuchanganya aina mbalimbali za dawa za kulevya.

"Unaweza kusikia mtu amefariki ghafla, kwa daktari kujua ni rahisi unauchana moyo, ukiufungua kuna mishipa mikubwa miwili mtu ambaye ameachanganya dawa mmoja wa mshipa unaweza kupasuka na kumsababishia kifo,".

Alichokisema Dk Nyandindi kinashabihiana na kauli ambayo iliwahi kutolewa na Mkurugenzi wa Tiba wa wizara ya afya Dk Grace Maghembe wakati wa ufunguzi wa maadhimisho ya wiki ya magonjwa yasiyoambukizwa Novemba mwaka jana.

Kulingana na Dk Maghembe takwimu zinaonyesha kwa takriban miaka minane magonjwa yasiyoambukiza yanatesa zaidi kundi la vijana na watoto tofauti na hapo kabla ambapo kundi la watu wazima ndilo lililokuwa likiugua.

"Zamani yaliaminika kuwa ya watu wazima, hata hivyo kwa miaka takriban minane yanaonekana kwa watoto na vijana ambao tunasema ndiyo kundi lenye nguvu na uwezo wa kuzalisha," anasema Dk Maghembe.

Uhusiano wa hili unakuja kutokana na ukweli kwamba watumiaji wa dawa za kulevya wengi ni vijana na huenda ndio wanaochangia katika ongezeko la watu wenye magonjwa yasiyoambukiza hapa nchini.